

**HALAMASHAURI YA JIJI LA ARUSHA**  
**MTIHANI WA PILI WA KUJISOMEA NYUMBANI**  
**DARASA LA NNE 2020**

**SOMO: SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

**JINA:** \_\_\_\_\_ **SHULE:** \_\_\_\_\_

**MUDA: SAA 1:30**

**JUNI, 2020**

**MAELEKEZO**

- i. Mtihani una jumla ya maswali matano (5)
- ii. Jibu maswali yote kwa usahihi .

**SEHEMU: A**

1. Chagua jibu sahihi katika machaguo uliyopewa kisha uandike herufi ya jibu sahihi mbele ya kisanduku kwa kila swali.
  - i. \_\_\_\_\_ husababisha mabapa ya kinu upepo kuzungushwa.
    - a)Jua linapowaka b)Taa zinapowashwa c)Upepo unapovuma d)Mvua inaponyesha ( )
  - ii. Chakula aina ya kabohaidreti hutupatia \_\_\_\_\_.
    - a) nishati b) joto c) maji d)vitamini ( )
  - iii. Jua husaidia kung'arisha nguo \_\_\_\_\_ .
    - a) za rangi isiyotoka b) zinazotoa rangi c) Nyeupe d) Nyeusi ( )
  - iv. Tunapopiga pasi nguo tunaanza sehemu za \_\_\_\_\_ .
    - a) ndani b) nje c) ukosini d) mikononi ( )
  - v. Anofesi hueneza ugonjwa wa \_\_\_\_\_
    - a) Kichocho b) Malaria c) Surua d) Kifua kikuu ( )
2. Linganisha **KIFUNGU A** na **KIFUNGU B** ili kupata maana kisha andika herufi ya jibu sahihi katika sehemu ya majibu.

	KIFUNGU A		KIFUNGU B
i	Kunywa dawa kiholela	A	Husababisha mafuriko
ii	Mlo kamili	B	Kinga isiyo ya asili
iii	Chanjo	C	Husababisha mwanga kupinda
iv	Mvua kubwa	D	Huhusisha makundi mbalimbali ya vyakula
v	Midia angav umbili	E	Hupunguza uwezo wa kinga kupambana na viini vya magonjwa.

KIFUNGU A	i	ii	iii	iv	v
KIFUNGU B					

3. Jaza sehemu zilizoachwa wazi kwa kuchagua jibu sahihi kutoka katika kisanduku hapo chini.


**Soketi ya umeme, Vimeng'anya, Kizingiti, Data, Jotoridi, Nyuzi joto, Swichi, Utumbo**

- i. Hali ya ubaridi au joto la kitu huitwa\_\_\_\_\_
- ii. \_\_\_\_\_ni kiwango kinachobainisha mpaka wa utokeaji wa badiliko la kiumbo la kitu.
- iii. \_\_\_\_\_ni kifaa chenye ncha mbili au tatu ukutani ambapo plagi ya umeme huhomekwa.
- iv. Taarifa zinazotokana na utafiti zinazotumika kuelezea au kuthibitisha jambo Fulani huitwa\_\_\_\_\_.
- v. \_\_\_\_\_ni kemikali zinazosaidia usagaji wa chakula tumboni.

4. Andika **NDIYO** kwa sentensi sahihi na **HAPANA** kwa sentensi isiyo sahihi.

- i. Mwili wa binadamu wenye afya una uwezo wa kupambana na vimelea vinavyosababisha magonjwa. \_\_\_\_\_.
- ii. Pepopunda ni ugonjwa usiosababishwa na bacteria. \_\_\_\_\_
- iii. Mtu asiye mwenye upungufu wa madini joto hupata na ugonjwa wa goita. \_\_\_\_\_
- iv. Friza ni sehemu katika jokofu ambayo mashine yake hugandisha barafu na vyakula.\_\_\_\_\_.
- v. Mkaa upo katika hali yabisi \_\_\_\_\_.

5. Taja majina ya sehemu zilizoandikwa herufi katika mchoro ufuatao wa sakiti rahisi ya umeme.



A) i) \_\_\_\_\_

D) iv) \_\_\_\_\_

B) ii) \_\_\_\_\_

E) v) \_\_\_\_\_

C) iii) \_\_\_\_\_